CRDB BANK

Tunakusikiliza

# NAFASI ZA UJUMBE WA BODI

CRDB Bank Plc ni benki ya kibiashara inayoongoza nchini Tanzania. Benki hii ilianzishwa mwaka 1996 na imekua na kuwa benki bora yenye ubunifu na inayoaminika zaidi nchini. Benki ilipata mafanikio makubwa baada ya kuorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam mnamo tarehe 17 Juni 2009. Benki ya CRDB inamiliki kampuni tanzu nne ambazo ni CRDB Bank Burundi *S.A., CRDB Insurance Company Limited, CRDB Bank Foundation na CRDB Bank DR Congo S.A.*

Bodi ya Wakurugenzi inakaribisha maombi kutoka kwa wagombea wenye sifa zinazofaa kujaza nafasi tano (5) za ujumbe wa Bodi kama ifuatavyo:

i. Mjumbe mmoja (1) huru wa Bodi kuwakilisha wanahisa wote

ii. Mjumbe mmoja (1) wa Bodi kuwakilisha kundi la wanahisa wanaomiliki hisa zaidi ya 1% na chini ya 10%.

iii. Wajumbe watatu (3) wa Bodi kuwakilisha kundi la wanahisa wanaomiliki hisa chini ya 1%.

- Wajumbe wote wa Bodi waliotajwa hapo juu watachaguliwa na Wanahisa kulingana na makundi yao ya umiliki wa hisa isipokuwa Mjumbe huru wa Bodi ambaye atachaguliwa na Wanahisa wote.
- Majina ya wagombea wenye sifa yatapelekwa kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 30 utakaofanyika tarehe 17 Mei 2025 kwa ajili ya uchaguzi.

**Elimu na Weledi**

Kwa mujibu wa kifungu cha 5(2) cha Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha (Utawala Bora) ya mwaka 2021, mgombea wa nafasi ya Mkurugenzi wa Bodi anatakiwa kuwa na weledi na elimu kwenye nyanja zifuatazo: benki; au utaalamu wa mambo ya fedha, au uhasibu; au ukaguzi; au Sheria; au Uchumi.

**Ujuzi na Utaalamu**

Kutokana na Muundo wa sasa wa Bodi, maendeleo ya teknolojia na kukua kwa utoaji wa huduma za kibenki kidijitali ujuzi ufuatao unahitajika: data science na Usalama wa Mtandao, Sheria, Uhasibu na Ukaguzi, Uhandisi, Teknolojia ya Habari (Uhandisi wa Programu, Teknolojia na Mifumo), Utawala wa Kijamii wa Mazingira (ESG) na Uendelevu, Rasilimali Watu, Utaalam wa Huduma za Bima na awe na uzoefu wa angalau miaka mitatu kwenye nafasi ya Ukurugenzi wa Bodi.

**Majukumu ya Bodi ya Wakurugenzi**

1. Kutoa muongozo juu ya maono, dhamira na miiko ya Benki yenye dhumuni la kuendeleza ustawi na uhai wa Benki.
2. Kusimamia na kutathimini Mikakati ya Benki kufanikisha Maono na Dhamira na kuhakikisha Benki inaendelea kuwepo na kustawi.
3. Kuisimamia benki kupitia sera na malengo mapana, yaliyoundwa na kukubaliwa na Mkurugenzi Mkuu. Sera na Malengo hayo yatahakikisha kuwa :
   - 3.1 Kunakuwepo na utaratibu na utendaji wa kulinda rasilimali na heshima ya Benki;
   - 3.2 Benki inazingatia sheria zote, kanuni na taratibu za utendaji bora;
   - 3.3 Teknolojia na mifumo inayotumiwa na Benki ni sahihi kwa ajili ya Benki kuwa na ushindani kwa kutumia vizuri rasilimali zake, michakato ya utendaji na rasilimali watu;
4. Kusimamia utambuzi wa vihatarishi na namna ya kuvidhibiti ili kukuza thamani ya hisa kwa muda mrefu;

**Utaratibu wa Kuwasilisha Maombi**

1. Mtu yeyote mwenye nia ya kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa bodi inabidi atume barua ya maombi, wasifu, nakala zilizo thibitishwa za vyeti vya shule/vyuo na taaluma na tuzo, picha mbili (passport size), nakala zilizothibitishwa za ukurasa wa mwisho wa hati ya kusafiria, barua kutoka kwa wadhamini watatu (3) na tamko la kutodaiwa na benki yoyote.
2. Taarifa ya kupokelewa kwa maombi pamoja na maelezo mengine yatatumwa kwa waombaji wote mara baada ya maombi kupokelewa. Mgombea aliyefanikiwa atahudumu kwa kipindi cha miaka 3 ambacho kinaweza kuongezwa. Maombi yote ni lazima yapokelewe **kabla ya saa kumi (10.00) jioni siku ya Ijumaa tarehe 28 Februari, 2025**.

**CRDB inahimiza wanawake wanaokidhi vigezo kuwasilisha maombi yao.**

Anuani kwa mawasiliano :

Katibu wa Benki,

CRDB Bank Plc Head Offices, Ali Hassan Mwinyi road

P.O. Box 268,

Dar es Salaam.

**Email: Boardmembers.Applications@crdbbank.co.tz.**

**Tel: +255 (0) 22 221 9566.**

**KWA IDHINI YA BODI**

Pascal T. Mihayo

**KATIBU WA BENKI**